**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA

# KUHUSU UTEUZI WA MBUNGE NA DIWANI MWANAMKE WA VITI MAALUMU

**Dodoma, 19 Januari, 2026**

Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 66(1)(b) na 78(1) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 112 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 19 Januari, 2026 imefanya uteuzi wa **Ndugu Zulfa Mmaka Omar** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Mbunge Mwanamke wa Viti Maalumu.

Nafasi hiyo imejazwa kwa kuzingatia matokeo ya Uchaguzi wa Marudio wa Ubunge katikati Jimbo la Fuoni kwa Tanzania Zazibar na Jimbo la Siha kwa Tanzania Bara.

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 25(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 kikisomwa pamoja na kifungu cha 113 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 19 Januari, 2026 imefanya uteuzi wa **Ndugu Amina Hussein Zihuye** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani Mwanamke waViti Maalumu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Uteuzi huo umefanyika baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa marudio katika Kata ya Mindu na Kata Chamwino katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambapo uchaguzi uliahirishwa kutokana na vifo vya baadhi ya wagombea katika kata husika.

Imetolewa na:

Kailima, R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**